**TAMKO LA TAPO LA WANAWAKE NA WASICHANA KULAANI KUUWAWA KWA MSICHANA NANYOLI**

Sisi tapo la watetezi wa haki za watoto, wasichana na wanawake tunalaani vikali kitendo cha msichana Nanyoli Mohee (22) wa kabila la Masai kuchapwa fimbo kikatili na mwanaume ambapo alipata majeraha ambayo hatimaye yalimsababishi kifo. Msichana huyo alifanyiwa ukatili huo kutokana na kukataa kuishi na mwanaume ambaye wazazi wa msichana huyo walitaka kumuozesha kwa nguvu, aliozeshwa mwezi Novemba 2023 kwa sababu alikuwa amelipiwa mahari na huyo mwanaume tangu akiwa mtoto mdogo. Binti huyo alikatkataa kulazimishwa kuolewa na alikimbia nyumbani kwa wazazi wake akawa anaishi porini. Lakini tarehe 06 Februari 2024 mtu mmoja anayemfahamu, alimkamata na kumrejesha nyumbani kwa wazazi wake na ndipo baba yake akampigia simu huyo mwanaume aliyetoa mahari Amyor Mathayo, Mmasai kutoka kijiji cha Endepes ili aje kumchukua aondoke naye. Binti huyo alipokataa huyo mwanaume alitafuta fimbo akamchapa kikatili mbele ya baba yake mzazi na kusababisha majeraha na maumivu makali sehemu mbalimbali za mwili wake. Kutokana na binti huyo kupiga mayowe kutokana na maumivu makali wanajamii waliosikia walikuja nyumbani kwa baba yake binti huyo wakamchukua na kumpeleka kwenye zahanati kupata matibabu. Lakini kutokana na kuumizwa vibaya mwili mzima asubuhi ya tarehe 07/02/2024 ilibidi apelekwe hospitali ya Malambo ambapo hali ilibadilika na kufariki dunia

Sisi tapo la watetezi wa haki za watoto, wasichana na wanawake, tumesikitishwa na kuumizwa na tukio hili la kikatili ambalo ni mwendelezo wa vitendo vya ukatili dhidi ya watoto, wasichana na wanawake kuuwawa unakoendelea katika sehemu mbalimbali nchini ambapo ni kinyume na sheria na Katiba ya Jamhuri ya muungano Tanzania.

Sisi tapo la watetezi wa haki za watoto, wasichana na wanawake tunauliza maswali yafuatayo:

- ➔ Je ni mpaka wauwawe watoto wangapi wa kike kwa kukataa kulazimishwa kuolewa katika umri mdogo ndipo Wizara ya Katiba na Sheria ione umuhimu wakuifanyia marekebisho ya Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 Bungeni ambayo ina kifungu cha 13 na 17 kinachoruhusu mtoto wa kike na umri wa chini ya miaka 15 kuolewa?
- ➔ Je ni mpaka lini Wabunge ambao ndio wawakilishi wa wananchi wataendelea kukaa kimya bila kuidai Serikali ipeleke Bungeni Muswada wa kuifanyia marekebisho Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971?
- ➔ Ni hadi wauwawe wasichana wangapi kwa kukataa kulazimishwa kuolewa ndipo wizara TAMISEMI ione umuhimu kuagiza serikali za Vijiji/Mitaa kuweka utaratibu wa kulinda watoto wa kike wasifanyiwe vitendo vya ukatili ikiwa ni pamoja na kulazimishwa kuolewa wakiwa bado watoto kwa sababu yoyote ile?
- ➔ Je ni hadi lini jamii zote katika maeneo yote ya Tanzania wataona umuhimu wa kuchukua hatua stahiki bila ucheleweshwaji ili kuepusha watoto wa kike kuumizwa na/au kuuwawa kwa sababu ya kulazimishwa kuolewa?

**MATUKIO YA WASICHANA WENYE UMRI MDOGO KULAZIMISHWA KUOLEWA YALIYORIPOTIWA HAPO NYUMA.**

Sisi tapo la watetezi wa haki za watoto, wasichana na wanawake tunauliza maswali hayo hapo juu kwa sababu yapo matukio ya mauaji yamewafika wasichichana wengine wenye umri mdogo katika sehemu mbali mbali nchini kwetu ambayo hayakuripotiwa na yapo ambayo yameripotiwa. Mfano wa matukio yaliyoripotiwa ni haya:

Kwa mfano matukio ya Mwaka 2022 ni haya yafuatayo:

- **Rebeca Benjamini** mkazi wa Mkoa wa Geita, Kata ya Izunya, Wilaya ya Nyang'hwale mwenye umri wa miaka 17 alijiua kutokana na msongo wa mawazo uliosababishwa na kulazimishwa kuolewa.. ''Rebeca amefariki dunia baada ya kujinyonga hadi kupoteza maisha kwa kutumia kamba iliyosukwa kwa chandarua kwenye kenchi ya nyumba yake, chanzo kikionesha alikuwa akilalamika kwamba kwanini kila akiolewa anaachika na tayari alikuwa aeshaachika mara tatu'' Henry Mwaibabe, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita.
- Kisa kingine kilitokea Mkoa wa Songwe, kijiji cha Ilanga, kata ya Mlale, pale mtoto wa kiume mwenye miaka 16 alipomuua mkewe wa miaka 16 kisha kumchoma moto na kumtupa kwenye korongo.
- Tukio lingine lilitokea Mkoa wa Kigoma, Kijiji cha Lufubu, Wilaya ya Uvinza, lililomuhusisha binti **Mbaru Juakali (**17) kulazimishwa kuolewa baada ya wazazi wake kupokea mahari ya ng'ombe 13, lakini alipokataa alipigwa fimbo na baba yake baadaye akapigwa na baba yake mkubwa hadi akafariki dunia.

## JITIHADA ZA WANATAPO KUPAZA SAUTI KUHUSU NDOA ZA UTOTO

Harakati za wana tapo zimekuwa na mafanikio kadhaa ikiwa ni pamoja na maamuzi ya mahakam**a** ya Rufaa ambapo iliielekeza Serikali kwamba ndani ya mwaka mmoja kubadilisha Sheria ya Ndoa inafanyiwa maboresha kuweka miaka 18 kama umri wa chini wa kuoa/kuolewa kwa wasichana na wavulana. Tunafahamu kwamba Serikali ikusuasua kutekeleza maamuzi hayo kama hukumu ilivyoelekeza, ni kuchochea kutozingstiwa kwa haki za watoto wa kike nchini.

Mwezi Septemba 2022, Serikali ilitoa kauli kuhusu mchakato wa mabadiliko ya sheria ya ndoa ya mwaka 1971, ili kutatua changamoto ya kukosekana kwa tafsiri moja ya kisheria ya umri wa mtoto kuoa na kuolewa.

Pia mwaka 2022,, tapo la wanawake na wasichana tulitoa tamko na kusisitiza kuhusu msimamo wetu, hasa kutokukubaliana na hatua ya kukusanya maoni ambayo tuliona pamoja na kuchelewesha utekelezaji wa hukumu, ni matumizi mabaya ya pesa za serikali, wananchi pamoja na wahisani katika suala hili. Pia tulisisitiza kitendo hiki cha kukusanya maoni kuwa ni kwenda kinyume na misingi ya utawala bora lakini pia, Bunge kama chombo kilichopewa dhamana ya kutekeleza maamuzi yaliyotolewa na mahakama linakuwa halijatimiza jukumu lake la kikatiba.

Mwaka 2023 mwezi wa Aprili Serikali chini ya Wizara ya Katiba na Sheria kupitia waziri wake walitoa tamko na kutuhakikishia jamii kuwa Sheria ya Ndoa itafanyiwa maboresho na haitakuwa na vikwazo vyovyote kauli hiyo ilitolewa na Waziri wa hiyo mbele ya jukwaa la Wakurugenzi Wanawake waliowakilisha mashirika ya haki za wanawake na wasichana nchini. **"Serikali ina nia ya kupeka muswada wa mabadiliko ya sheria ya ndoa 1971 katika Bunge hili la bajeti linalondelea ili kuweka umri wa miaka 18 kama umri wa chini wa kuolewa na kuoa", alisema -** Mh. Dr. Damas Ndumbaro –Waziri wa Katiba na Sheria mwaka jana 2023.

## KWANINI MATUKIO HAYA YANAENDELEA NCHINI?

Sheria zetu bado zinaruhusu ndoa za utotoni kuendelea hasa kifungu 13 na 17 ya sheria ya Ndoa ya mwaka 1971. Ikumbukwe pia kuwa Mahakama katika shauri la *Rebeca Gyumi* iliamuru Serikali kufanya

marekebisho ya sheria ndani ya mwaka mmoja na kusahihisha vifungu vya kibaguzi vya 13 na 17 na kuweka miaka 18 kama umri wa chini unaostahili kwa ndoa kwa wavulana na wasichana. Mahakama katika kujielekeza kwenye maamuzi ya umri wa miaka 18 ilizingatia mambo mengi ikiwemo sababu za kisheria na kisera Kwa hiyo, serikali inawajibu pia wa kutekeleza maelekezo ya Mahakama kuhusu umri wa chini mtu (mwanamke au mwanaume ) kuingia kwenye ndoa.

Hali kadhalika, Serikali hadi sasa haijaonesha nia ya kisiasa (political will) katika kushughulikia ndoa za utotoni kama kutekeleza mikataba ya kimataifa na ya kikanda ya haki za binadamu; mfano SADC Model Law to Eradicate Child Marriage, Convection on the Rights of the child e.t.c.

Kuwepo kwa mihanya na mwanya kwenye eneo la ushahidi pamoja na uchunguzi wa kesi kwenye mifumo ya kutoa Haki mfano Mahakama, Polisi,Viongozi wa serikali ya mitaa na Halmashauri walitweza jukumu la ulinzi wa watoto. ambapo kesi nyingi sana zinekuwa zinakuwa haziendeshwi hadi mwisho kutokana na kukosa ufuatiliaji sahihi wa matukio.

**KAULI YETU**

Ni muhimu ieleweke kuwa, bila kuchukua hatua sahihi watoto wetu watazidi kufanyiwa ukatili wa kijinsia na kupoteza maisha yao.Hivyo basi, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndio mhimili wenye jukumu la kutunga sheria na kufanya marekebisho ya sheria hivyo basi lina wajibu wa kufanya mabadiliko ya Sheria ya Ndoa ya nwaka 1971.

Serikali kuharakisha mchakato wa mabadiliko ya vifungu vya 13 na 17 vya Sheria ya Ndoa, 1971 kama ilivyoamriwa na mahakama ya rufaa katika Shauri la Rebeca Gyumi dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali Katika Shauri la Madai Na.5 ya 2016.

Vilevile serikali ya wilaya ya eneo husika ambapo mauaji na ukatili huu wa kinyama umefanyika , ichukue hatua kali za kisheria dhidi ya wazazi, mtuhumiwa na yeyote atakaebainika amehusika kwa namna moja au nyingine ili iwe fundisho kwa wazazi wanao waozesha watoto na wanajamii chukua sheria mkononi na kukatisha maisha ya wengine.Tunaamini "**UHAI WA MTU YEYOTE UNATHAMI NIWA"**

Wanatapo tunatoa pendekezo kwa mamalaka husika kuchukua kesi hizi kwa umakini na kuhakikisha uchunguzi unafanyika aidha kwa kuunda tume yenye mamlaka ya kuchunguza kesi hizi za ukatili zilizo ripotiwa.

**Tunadai uwajibikaji.**

**HITIMISHO**

**Sisi kama tapo watetezi wa haki za watoto, wasichana na wanawake wa Tanzania tunadai mambo yafuatayo;**

1. Mwili wa binti huyo usizikwe mpaka mwili wake ufanyiwe uchunguzi wa kidaktari na ripoti ya uchunguzi huo ikabidhiwe kwa vyombo vinavyohusika kisheria.
2. Vyombo vya ulinzi na usalama yani Polisi na Madawati ya Kijinsia yatekeleze majukumu yake kikamilifu na kwa uadilifu katika kushughulikia kesi hadi mwisho.

3. Wabunge kupitia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakitekeleze jukumu lao la kikatiba la kuitaka Serikali ilete mswada kwa ajili ya mabadiliko ya Kifungu cha 13 na 17 cha Sheria ya Ndoa, 1971 .
4. Serikali ichukue hatua kali dhidi ya hizi kesi za ukatili na kuboresha mifumo, upelelezi wa kesi, dhamana, na ufuatiliaji.

**Tunatoa wito kwa Serikali kuharakisha inachukua hatua za kukomesha ndoa za utotoni na kuwalinda wasichana wetu dhidi ya unyanyasaji wa kingono na kijinsia.**

**Imetolewa na wana tapo la watetezi wa haki za watoto, wasichana na wanawake mnamo tarehe tarehe 09/02/2024**

**Saini………………………………..**

**Mwenyekiti wa tapo la watetezi wa haki za watoto, wasichana na wanawake**